

Jina.....

Nambari yako...../.....

Shule.....

Tarehe .....

Sahihi ya Mtahiniwa.....

102/3

**KISWAHILI**

**Karatasi ya 3**

**(FASIHD)**

**JULAI / AGOSTI - 2012**

**MUDA: SAA 2 ½**

**MTIHANI WA TATHMINI WA PAMOJA WA WILAYA YA KWANZA- 2012**  
**Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari**

**Maagizo**

1. Jibu maswali MANNE pekee
2. Swali la kwanza ni la LAZIMA
3. Chagua maswali mengine matatu kutoka sehemu zilizosalia
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
5. Kila swali lina alama 20

*Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa*

*Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa*

## SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

1. Swali la lazima
  - a) Eleza wahusika aina tano wa fasihi simulizi. (Alama 10)
  - b) Eleza sifa za wahusika wa mighani. (Alama 10)

## SEHEMU YA B: TAMTHILIA (Kifo Kisimani na Kithaka Wamberia)

### Jibu swali la 2 au 3

2. “Bizo ndizo athari za utawala mbaya huwageuza binadamu kuwa wanyama kasoro mkia na masikio marefu”
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)
  - b) Fafanua maudhui yoyote manne yanayorejelewa katika dondoo hili. (Alama 8)
  - c) Eleza athari zozote tatu za utawala mbaya kwa wanabutangi. (Alama 8)
3. “Mwandishi wa tamthilia ya Kifo Kisimani anapigana dhidi ya kukosekana kwa haki.” Jadili. (Alama 20)

## SEHEMU YA C: RIWAYA (Utengano na S.A Mohamed)

### Jibu swali la 4 au 5.

4. “Malezi ya motto wa kike ni kizungumkuti”. Thibitisha kwa kutoa mifano mwafaka kutoka katika Riwaya ya Utengano. (Alama 20)
5. “Mara ngapi kakangu nimekuwasa juu ya mwendo wako? Lakini .....”
  - a) Eleza muktadha wa dondoo. (Alama 4)
  - b) Kwa kurejelea dondoo hili, eleza sifa za mzungumzaji (Alama 6)
  - c) Kwa kurejelea wahusika katika dondoo, eleza jinsi suala la uwajibikaji unavyojitokeza. (Alama 10)

## SEHEMU YA D: USHAIRI

### Jibu swali la 6 au 7

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata
  - a) Ni sumu, sumu hatari  
unahatarisha watoto

kwa ndoto zako leweshi

za kupanda ngazi,

Ndoto mototo ambazo

Zimejenga ukuta

Baina ya watoto

Na maneno laini

Ya ulimi wa wazazi

b) Ni sumu, sumu hasiri

Unahasiri watoto

Kwa pupa yako hangaishi

Ya kuwa tajiri mtajiriko,

Pupa pumbazi ambayo

Imezaa jangwa bahili

Badala ya chemichemi

Ya mazungumzo na maadili

Baina ya watoto na mzazi

c) Ni sumu, sumu legezi

unalegeza watoto

kwa mazoea yako tetanishi

Ya daima kunywa 'maji baridi'

Mazoea mabaya ambayo

Yanakufunga katika klabu

Hadi saa nane usiku

Huku yakijenga kutofahamiana

Baina ya watoto na mzazi

- d) Ni sumu, sumu jeruhi  
unajeruhi watoto kwa pesa  
kwa mapenzi yako hafari  
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa  
Zinawafikisha kwenye sigara na ulevi  
Na kisha kwenye madawa ya kulevyo  
Barabara inayofikisha kwenye giza baridi  
La kaburi la asubuhi

### Maswali

- a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili. (Alama 1)
- b) Fafanua maudhui ya shairi hili. (Alama 4)
- c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta. (Alama 2)
- d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uzitolee mifano. (Alama 4)
- e) Eleza umbo la shairi hili. (Alama 3)
- f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha nathari. (Alama 4)
- g) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi. (Alama 2)
- i) Giza baridi
- ii) Yanakufunga katika klabu

### HADITHI FUPI: MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINE

7. Mizozo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ni chanzo kikuu cha ukosefu wa amani katika nchi nyingi za Afrika mashariki. Dhihirisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea madhara ya vita vya kikabila na suluhu yake kwa mujibu wa Mkimbizi na Johnn Habwe. (Alama 20)

For More Free KCSE past papers visit [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)

**MWISHO**